

HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Arusha,
Telegram: Arusha.
Simu: 073 6500476,
Faksi: 250 3701.
Email:ded@arushadistrict.go.tz



Ukumbi wa Wilaya,
S. L. P. 2330,
ARUSHA.

www.arushadc.go.tz

MPANGO KABAMBE WA JIJI LA ARUSHA 2035. ARUSHA 2035 MASTER PLAN

Mpango kabambe wa Jiji la Arusha unatekelezwa na Serikali Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na serikali ya Singapore. Mpango huu unajulikana kama **Arusha City Master Plan 2035**.

Katika Tanzania Mpango huu unatekelezwa kwenye majiji mawili ikiwemo Jiji la Arusha na Jiji la Mwanza na ulianza mwaka 2014 kwa kufanya tafiti mbali mbali juu ya Ardhi na Makazi na ni mpango wa muda mrefu mpaka mwaka 2035.

UTANGULIZI NA HISTORIA FUPI.

Mwaka 2014 Serikali kupitaia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi ilisaini Mkataba wa makubaliano na Serikali ya Singapore (MoU) kutekeleza miradi ya kuendeleza miji na uandaaji wa Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha na Mwanza.

Kazi hiyo inafanywa na Singapore Cooperation Enterprises kwa kushirikiana na Surbana International Consultant Pte. Kazi hiyo ya uandaaji wa Mpango Kabambe ilianza mwezi Februari , 2015 na inategemea kukamilika mwezi Agosti, 2016.

Mikutano ya kitaifa ikihusisha taasisi mbalimbali za serikali

Katika hatua za kutekeleza Mpango kabambe mikutano Mbalimbali ya kitaifa ilifanyika jijini Dar Es Salaam iliyohusisha taasisi mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
- Bodi ya Taifa ya Utalii
- Wizara ya Kazi na Ajira
- Baraza la hifadhi ya Mazingira
- TANROADS
- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa
- Wizara ya Maliasili na Utalii
- Shirika la Maendeo ya Taifa
- Idara ya Mipangomiji na Vijiji
- Shirika la Nyumba la Taifa
- Idara ya Umipaji na Ramani - Wizara ya Ardhi

Picha ya Mkutano wa wadau wa kitaifa kuhusu Mpango Kabambe.



Eneo lililotangazwa kuwa mji kwa ajili ya kuandaliwa Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha lina ukubwa wa Kilomita za mraba 608, linahusisha eneo lote la Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya halmashauri za Wilaya za Arusha na Meru.

Mpango Kabambe wa Jijij la Arusha unalenga kulifanya Jiji la Arusha pamoja na Viunga Vyake ikiwa ni eneo lote la Jiji na Arusha na Baadhi ya maeneo katika Halmashauri ya Meru na Arusha kuwa sehemu nzuri ya kuishi na ya kuvutia ifikapo mwaka 2035.

Maboresho yanalenga katika kupanga Jiji na kuboresha maeneo ya makazi, Biashar na viwanda pamoja na kuimarisha miundombinu sambamba na upatikanaji wa huduma za jamii.

Mpango kabambe wa Jiji la Arusha unalenga kupanga Mji wa Arusha kwa kuzingatia maeneo halisi, Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, ukuaji wa kasi wa miji, maeneleo ya kiuchumi, mahitaji ya jamii pamoja na ongezeko la watu katika ardhi hii isiyoongezeka.

Mpango Kabambe unalenga pia kuinua hali ya ya maisha ya watu kwa kujenga mji wa kiteknolojia (smart city) kwa kuboresha matumizi sahihi ya ardhi, miundombinu na usafirishaji.

Jiji la Arusha ni kitovu cha shughuli za kidemokrasia, kiutamaduni, na kielimu pia ni kitovu cha utalii na inajulikana kama kituo kikuu cha shughuli za utalii hapa nchini kutokana na kuwa na mbuga za asili na vivutio vya utalii vinavyofahamika kote ulimwenguni.

Arusha pia ni makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Arusha inauwezo wa kuwa jiji kuu la Afrika Mashariki lenye uwezo wa kuleta maendeleo katika mkoa wa Arusha na nchi ya Tanzania kwa ujumla.

Arusha pia inajulikana kama jiji la kijani kutokana na wingi wa uoto wa asili na kuwa na ardhi yenye rutuba. Arusha inachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Tanzania kupitia utalii, kilimo na madini na ni lango kuu la kuingilia katika fursa na vivutio mbalimbali vilivyopo kaskazini mwa Tanzania.

Fursa zote hizi zimefanya Jiji la Arusha kuwa mji muhimu Tanzania na hivyo kupelekea kupendekezwa kwa dira ya Jiji la Arusha 2035.

Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha unajumuisha Halmashauri yote ya Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo katika Halmashauri ya wilaya ya Meru na Halmashauri ya wilaya ya Arusha.

Eneo hilo la Mpango Kabambe lenye ukubwa wa kilomita za mraba 608 limezingatia hali halisi ya ukuaji wa Jiji pamoja na Viunga vyake na mwelekeo wake baadaye huku kukiwa na msisitizo wa kuzuia mtawanyiko wa Jiji, na kuzuia uharibifu wan a kutunza Bioanuai inayozunguka Jiji la Arusha. Mipaka ya eneo la Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha umetanda kuanzia Kisongo na Ngaramtoni kwa upane wa Magharibi hadi Maji ya chai na Kitovu kwa upande wa Mashariki

Katika Halmashauri ya Arusha Mpango kabambe wa Jiji la Arusha unategemea kutekelezwa katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 149 kwenye baadhi ya maeneo katika kata za Oloirieni, Kimnyaki, Bangata, Moivo, Mlangarini, Kiranyi, Kiutu, Sokoni II, Ilboru na Matevesi.

Mpango huu umepanga maeneo ya makazi, maeneo ya huduma za Jamii kama shule, viwanja vya wazi, maeneo ya Viwanda, maeneo ya Kilimo na mifungo, maeneo ya biashara ndogo ndogo n.k.

Picha ya Mkutano wa wadau wa kitaifa kuhusu Mpango Kabambe.



Eneo lililotangazwa kuwa mji kwa ajili ya kuandaliwa Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha lina ukubwa wa Kilomita za mraba 608, linahusisha eneo lote la Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya halmashauri za Wilaya za Arusha na Meru.

Mpango Kabambe wa Jijij la Arusha unalenga kulifanya Jiji la Arusha pamoja na Viunga Vyake ikiwa ni eneo lote la Jiji na Arusha na Baadhi ya maeneo katika Halmashauri ya Meru na Arusha kuwa sehemu nzuri ya kuishi na ya kuvutia ifikapo mwaka 2035.

Maboresho yanalenga katika kupanga Jiji na kuboresha maeneo ya makazi, Biashar na viwanda pamoja na kuimarisha miundombinu sambamba na upatikanaji wa huduma za jamii.

Mpango kabambe wa Jiji la Arusha unalenga kupanga Mji wa Arusha kwa kuzingatia maeneo halisi, Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, ukuaji wa kasi wa miji, maeneleo ya kiuchumi, mahitaji ya jamii pamoja na ongezeko la watu katika ardhi hii isiyoongezeka.

Mpango Kabambe unalenga pia kuinua hali ya ya maisha ya watu kwa kujenga mji wa kiteknolojia (smart city) kwa kuboresha matumizi sahihi ya ardhi, miundombinu na usafirishaji.

Jiji la Arusha ni kitovu cha shughuli za kidemokrasia, kiutamaduni, na kielimu pia ni kitovu cha utalii na inajulikana kama kituo kikuu cha shughuli za utalii hapa nchini kutokana na kuwa na mbuga za asili na vivutio vya utalii vinavyofahamika kote ulimwenguni.

Arusha pia ni makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Arusha inauwezo wa kuwa jiji kuu la Afrika Mashariki lenye uwezo wa kuleta maendeleo katika mkoa wa Arusha na nchi ya Tanzania kwa ujumla.

Arusha pia inajulikana kama jiji la kijani kutokana na wingi wa uoto wa asili na kuwa na ardhi yenye rutuba. Arusha inachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Tanzania kupitia utalii, kilimo na madini na ni lango kuu la kuingilia katika fursa na vivutio mbalimbali vilivyopo kaskazini mwa Tanzania.

Fursa zote hizi zimefanya Jiji la Arusha kuwa mji muhimu Tanzania na hivyo kupelekea kupendekezwa kwa dira ya Jiji la Arusha 2035.

Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha unajumuisha Halmashauri yote ya Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo katika Halmashauri ya wilaya ya Meru na Halmashauri ya wilaya ya Arusha.

Eneo hilo la Mpango Kabambe lenye ukubwa wa kilomita za mraba 608 limezingatia hali halisi ya ukuaji wa Jiji pamoja na Viunga vyake na mwelekeo wake baadaye huku kukiwa na msisitizo wa kuzuia mtawanyiko wa Jiji, na kuzuia uharibifu wan a kutunza Bioanuai inayozunguka Jiji la Arusha. Mipaka ya eneo la Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha umetanda kuanzia Kisongo na Ngaramtoni kwa upane wa Magharibi hadi Maji ya chai na Kitovu kwa upande wa Mashariki

Mpango kabambe wa Jiji la Arusha unategemea kutekelezwa katika Halmashauri ya Arusha kwa eneo la kilomita za mraba 149 katika baadhi ya maeneo ya kata za Oloirieni, Kimnyaki, Bangata, Moivo, Mlangarini, Kiranyi, Kiutu, Sokoni II, Ilboru na Matevesi.

Mpango huu umepanga maeneo ya makazi, maeneo ya huduma za Jamii kama shule, viwanja vya wazi, maeneo ya Viwanda, maeneo ya Kilimo na mifungo, maeneo ya biashara ndogo ndogo n.k.

MPANGO UTAKUWA NA NINI?

Mpango Kabambe utakuwa na mambo yafuatayo:-

- Utakuwa na Ramani inayoonyesha hali halisi
- Taswira ya mpango
- Mapendekezo ya mpango wa matumizi ya ardhi
- Ramani mahsusi zinazoonyesha miundombinu mbalimbali kama barabara, maji, maji taka n.k
- Ripoti za mpango kabambe;
- Illustrative 3D Model inayoonesha sehemu ya eneo la katikati ya Jiji.
- Kuwa *website* (Mtandao) wa mpango kabambe kwa ajili ya matumizi ya umma na kuwa na uwezo wa kupakua (*download*) ramani


UCHAMBUZI WA ENEO LA MPANGO, HALI HALISI NA MAPENDEKEZO YA RASIMU YA MPANGO KABAMBE.

Jiji la Arusha: km sq 272

Wilaya ya Arusha: km sq 149

Wilaya ya Meru: km sq 187

Jumla ya Eneo la Mpango: km sq 608



Eneo la mpango ni 25% ya Arusha yote.

MPANGO KABAMBE UMEPANGA MATUMIZI YA ARDHI KAMA INAVYOONYESHA KWENYE RAMANI.


Makazi

Matumizi maalum


Viwanda

Biashara

Maeneo ya wazi



MUUNDO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO KABAMBE.



HATUA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO KABAMBE WA JIJI LA ARUSHA 2035

Stage 1

Inception &

Base mapping

Stage 2 : Preliminary-

Visioning &
Programming

Stage 3

Concept Plan for the City

Stage 4

Draft Master Plan & Zoning Plan

Stage 5 & 6

Final Master plan,
UD &
Implementation
Plan

Stage 7 & 8

Handholding (overlap with stage 7)

MP Launch

MIKUTANO MBALIMBALI YA WADAU ILIYOFANYIKA KATIKA MPANGO KABAMBE WA JIJI LA ARUSHA UKIJUMUISHA HALMASHAURI ZA JIJI LA ARUSHA, MERU NA ARUSHA.



MIKUTANO MBALI MBALI YA WADAU KATIKA HATUA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO KABAMBE WA JIJI LA ARUSHA 2035



MAWASILISHO YA RASIMU YA MWISHO YA MPANGO KWA WADAU.

Mkutano wa kuwasilisha Rasimu ya Mwisho wa mpango kwenye mkutano wa wataalamu na wadau wa Maendeleo kutoka halmshauri za Jiji la Arusha, Halmshauri ya Arusha na Halmshauri ya Meru.



MIKUTANO MBALIMBALI YA WADAU ILIYOFANYIKA KATIKA MPANGO KABAMBE WA JIJI LA ARUSHA UKIJUMUISHA HALMASHAURI ZA JIJI LA ARUSHA, MERU NA ARUSHA.



MIKUTANO MBALIMBALI YA WADAU KATIKA HATUA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO KABAMBE WA JIJI LA ARUSHA 2035.



MAWASILISHO YA RASIMU YA MWISHO YA MPANGO KWA WADAU.

Mkutano wa kuwasilisha Rasimu ya Mwisho wa mpango kwenye mkutano wa wataalamu na wadau wa Maendeleo kutoka halmshauri za Jiji la Arusha, Halmshauri ya Arusha na Halmshauri ya Meru.



MIKUTANO YA WANANCHI WA KUTOA MAONI JUU YA RASIMU YA MPANGO KABAMBE WA JIJI LA ARUSHA 2035.

Mkutano wa wananchi wa wananchi wa kijiji cha Mlangarini wa kutoa maoni ya Rasimu ya Mpango wa Jiji la Arusha 2035.



**MIKUTANO YA WANANCHI WA KUTOA MAONI JUU YA RASIMU YA MPANGO KABAMBE WA
JIJI LA ARUSHA 2035.**

Mkutano wa wananchi wa kijiji cha Sasi kata ya Bangata kwa ajili ya kutoa maoni ya Rasimu ya Mpango wa Jiji la Arusha 2035.



Mpaka kufikia tarehe 15.03.2017 hatua ya kutoa maoni ya wadau mbali mbali ikiwemo wananchi wa maeneo ambayo yameingizwa kwenye Mapango Kabambe wamemaliza kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha 2035.

Rasimu hiyo imerudishwa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya marekebisho kufuatia maoni yaliyotolewa na wadau mbali mbali.